

**KANISA KATOLIKI JIMBO KUU LA DAR ES SALAAM  
PAROKIA YA MT. MARIA DE MATTIAS – MIVUMONI  
DAR ES SALAAM**

---

**MATANGAZO YA DOMINIKA YA 28  
MWAKA C TAREHE 9 OCTOBA, 2022.**

**Kristo...**

**MCHANGO WA PILI**

Kwa ajili ya **UJENZI WA OFISI**. Jumuiya iandae vyombo, kwaya mtuongoze kwa wimbo.

**NDOA**

Bw. Florence Furaha mtoto wa Laurent Temba na Gloria Salim na Bi. Agness Kalisa mtoto wa Kalisa Blasio Kyaruzi na Shelestina Kamanzi.

**Tangazo la kwanza.**

Bw. Paulo Samson Marwa Mtoto wa Samson Chacha na Christina Matinde na Bi. Pendo Joseph Siong'o Mtoto wa Joseph Siong'o na Rhobi Ngoko.

**Tangazo la Pili.**

Anayejua kizuizi cha Tangazo hili atoe taarifa ofisi ya mapadre.

**UCHAGUZI WA VIONGOZI WA HALMASHAURI YA WALEI KATOLIKI**

Jana tarehe 8/10/2022 ilikuwa zamu ya jumuiya zilizobaki ambazo ni Mt. Petro, Mikael, Yuda Thadei, Martin de Porres, Faustina, Yohane Vianney, Maria Magdalena na Stephano Shahidi.

**HIJA UWAKA JIMBO**

Uongozi wa uwaka Parokia unawaomba viongozi wa Jumuiya kuratibu zoezi la kuandikisha mahujaji tarehe 14/10/2022 huko visiga kwa masista wa dada wadogo. Mwisho wa kuwasilisha majina utakuwa leo tarehe 9/10/2022 saa 12 jioni.

**SEMINA**

**WAWATA** Dekania ya Gasper na Thomas More wameandaa Semina kwa Watoto hasa watakaokuwa wamemaliza darasa la saba mwaka huu na Watoto wote kati ya miaka 11-16 itakayofanyika Bunju Parokiani siku ya tarehe 14/10/2022 Nyerere day. Gharama ni sh. 5000 ya kujikimu siku hiyo. Sote tunakaribishwa kuunga mkono siku hii muhimu kwa Watoto. Mada ni :

1. Kujitambua
2. Matumizi ya mitandao
3. Ushauri
4. Maungamo
5. Ibada ya Misa Takatifu.

Muda ni saa 3:00 Asubuhi.

Mwisho wa kupokea mchango ni tarehe 13/10/2022

**UZINDUZI WA KWAYA YA MT. YOHANE PAULO WA II**

Kwaya ya Mt. Yohane Paul ii ya hapa Parokiani inatarajia kufanya uzinduzi mkubwa wa Albam yake mpya iitwayo "Mwalimu wangu" iliyo katika mfumo wa video na

audio, siku ya jumapili ya tarehe 23/10/2022.Uzinduzi utafanyika katika misa zote mbili (ya kwanza na ya pili.Waumini wote tunakaribishwa kuwaunga mkono katika kuinua kazi hii nzuri ya kumtangaza Kristu kwa njia ya uimbaji.

(kumkaribisha mwana kwaya mmoja aliyeandaliwa aje aseme machache)

### **ST GASPER VOCATION TRAINING**

Wamisionari wa Shirika la Damu Aziz ya Yesu wanatangaza nafasi za masomo katika chuo chao cha Mt. Gaspar kwa fani za Electrical Installation, Information Technology, Motor vehicle Mechanics,Carpentry,Tailoring and design, Catering,Driving na English course kwa maelezo Zaidi fika ofisi ya H/walei Parokia.

### **UFADHILI WA MAFUNZO YA PRE FORM ONE**

Kituo cha Kein Open School kilichopo Madale kinatoa ufadhili kwa wanafunzi wawili (wakike na kiume) kwa ajili ya kusoma kozi ya Pre form one.Kozi hii ni kwa wanafunzi waliohitimu darasa la saba 2022.Kwa maelezo Zaidi fika ofisi ya Parokia.

### **UJENZI**

Tunaendelea na kazi ya plasta eneo la nje ya jengo la ofisi kazi hiyo inategemewa kukamilia ndani ya mwezi huu.

### **USAFI WA MAKABURI**

Kutakuwa na zoezi la usafi wa makaburi Jumamosi ya tarehe 22/10/2022 saa 12:30 Asubuhi, Kanda ya Nazareti, Bethsaida na Kapernaum watafanya usafi makaburi ya kwa Mponda.Kanda ya Yerusalemu, Bethlehemu,Kana, Galilaya na Bethania watafanya usafi makaburi ya Hope.Tuje na vifaa vya usafi kama vile mapanga, fyekeo, reki ,jembe na pia tuje na rosali na sadaka.

### **WAWATA**

Kutakuwa na kikao cha Halmashauri WAWATA Parokia itakayofanyika Dominika ijayo mara baada ya misa ya kwanza katika ukumbi wa Parokia.Walengwa ni viongozi wote watano wa kila jumuiya na watano wa wawata Parokia.Hivyo viongozi wote mnaombwa kusali misa ya kwanza ili kuweza kushiriki kikao hicho.

### **HUDUMA KANISANI**

Leo tunahudumiwa na Jumuiya ya Mt. Yohane Paul ii Dominika ijayo tutahudumiwa na Jumuiya ya Mt. Teresia wa Mtoto Yesu Wakati huohuo Jumuiya ya Mt. Yohane 23 wajiandae

### **MAUZO**

Gazeti la Tumaini letu linapatikana kwenye duka la WAWATA kwa shilingi 1,000 tu.Jipatie nakala yako ilio sheheni habari kemkem.